# HATUA KUMI (10) ZA MATESO ALIYOPITIA YESU ILI SISI TUPATE KUSAMEHEWA DHAMBI ZETU NA KUKUBALIKA MBELE ZA MUNGU BABA (GHARAMA ALIYOLIPA)

## A. UTANGULIZI

**Kila Mteule akielewa gharama aliyolipa Yesu ili tupate wokovu, hatauchezea wokovu kamwe**.

1. ***Math. 26: 36 – 46 (luk. 22: 40 – 46***) - Hatua ya kwanza ya mateso ya Yesu ya kimwili na Kiroho ilianzia katika bustani ya Gethsemane wakati akiomba. Yesu alifahamu kwa dhati kabisa mambo yanayokwenda kumpata; mambo ambayo mwili usingependa uyapitie ikiwa ni pamoja na adhabu ya kutengwa na Mungu Baba, adhabu ambayo ndiyo ya mwisho kwa watenda dhambi; ndiyo sababu aliomba hadi mishipa yake midogo ya kupitisha jasho ikapasuka na kuchanganyika na damu!!! Ni baada ya maombi haya ya mateso makubwa ndipo sasa anakuwa tayari kukubali mauti ya mwili pamoja na kukubali kutengwa kiroho na Mungu Baba yake wa Mbinguni ili aweze kufanikisha zoezi zima la wokovu wetu. ***Math. 27: 45 – 46***

   **Vs. 37:** ***"Yesu alihuzunika na kusononeka" he began to show grief and distress of mind and was deeply depressed***"

   **Yesu alianza kuonyesha hali ya huzuni na kuhangaika (na kulemewa/kutaabika katika nia/dhamiri yake na akaanza kwa kina sana kudhoofika/kusikitika kutokana na hali aliyokuwa anaenda kukabiliana nayo uso kwa uso. Isaya 53:3.**

***Note:*** **Haijawahi kutokea tangu Agano la Kale lote hadi Agano Jipya kuwapo Nabii au Mtume au Mchungaji au Mwinjilisti au Mwalimu, au Mwombaji yeyote ambaye amewahi kuomba hadi mishipa yake ya kupitisha jasho ikapasuka na kuchanganyika na damu!!! Mimi nilifika pale Gethsemane na kuonyeshwa alama ya kiganja chake kilichokuwa kimejaa damu kwenye jiwe pale aliposhika ili asianguke chini sababu ya uchovu**. **Hakika Yesu alilia kilio cha uchungu zaidi ya mtu yeyote duniani.** ***Ebr. 5: 7 - 8***

2. **<u>Hatua ya pili; Math. 26: 67- 68-</u>** Yesu alifungwa kwanza leso machoni pake, akatemewa mate usoni; akapigwa makonde, na wengine wakampiga makofi!!

- Kupiga makonde mtu aliyefungwa leso usoni si unapiga unavyotaka maana hawezi kuwepa!!!. ***Isay. 50:6***- Kila mteule apate picha hii akilini mwake. **Makonde** ni ngumi nzito sana.

3. **<u>Hatua ya tatu: Math. 27: 1 – 2</u>**. Yesu anapelekwa kwa Pilato akiwa amefungwa (Pilato alisifika kwa sifa mbili kubwa (alikuwa ni jeuri/katili, lakini pia alikuwa amejaa roho ya maringo na kiburi na kujivuna. ***Pilate was a man of a rough and haughty spirit. Math. 27: 11 – 14 na Yoh. 18: 29 -38***: Kiburi chake na jeuri yake Pilato alikwama kwa Yesu kabisa!!! Hili ni somo la ajabu sana, hata kama tumefikwa na changamoto nzito kiasi gani lazima tuwe na majibu yanayomwinua Mungu wetu***. Ayub. 19: 25 – 27, (Ayub. 1: 20 – 22, 2:10)***

4. **<u>Hatua ya nne ya mateso makali ya Yesu ni</u>** ***Math.27:26.*** Yesu anapigwa na mijeredi"

- **<u>Ngoja niwaambia kidogo kuhusu kupigwa kwa mijeledi</u>**

a. Mtuhumiwa alikuwa anavuliwa nguo zote kabla ya kuanza kupigwa.
b. Mtuhumiwa anafungwa kwenye mti mfupi (nguzo fupi) anafungwa mikono na miguu) ili akipigwa asijitetee
c. Mjeledi ulikuwa ni mkanda wa ngozi wenye kushonewa vipande vya chuma kikali mwishoni.
d. Yesu alipigwa na askari 2 wa Kirumi wakitumia mijeledi 2 hadi yalipofika mapigo **40- Kumb. 25: 1-3, (Paulo yeye alipigwa mapigo 39. 2Kor. 11: 24**
e. Kipigo hiki ndicho kilichopelekea mwili wa Yesu kukatwakatwa na mishipa ya vena na ateri ilitoa damu sana jambo ambalo inasadikika kuwa ndilo lililofanya Yesu Kristo aishiwe nguvu za kubeba msalaba aliotwishwa baadae. ***Luk. 23: 26.***
f. Wahalifu wengine walikuwa wakipigwa na mijeledi namna hii, viungo vya ndani kama utumbo, moyo, ini, mapafu vilikuwa vinatoka nje na walikukwa wanakufa wakati wakipigwa.

Ndiyo sababu Isaya alikuwa ametabiri kwamba uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mtu yeyote, na umbo lake zaidi ya wanadamu. ***Isaya. 52: 14***

5. H**<u>atua ya tano. Math. 27: 27- 31.</u>** Mwanzi (kama kofia hivi) waliomvisha Yesu kichwani ulikuwa na miiba; ndiyo sababu walipoupigapiga ukaingia kichwani!! Na ile miiba ilikuwa na aina fulani ya utomvu wenye sumu; hakika haya yalikuwa ni maumivu mengine makali sana yaliyosambaa mwili mzima!!! Lengo la kuvikwa kofia hii ya mwanzi kichwani na kuipigapiga ili iingie

ndani ni kumfanya Yesu **achanganyikiwe** na **kuvurugikiwa kiakili ili aanze kuropoka na kusema hovyo hovyo tu**. Hatusomi katika Biblia kama kuna mhalifu mwingine aliyewahi kuvikwa kofia hii ya miiba, hata wale wahalifu wawili waliosulubiwa na Yesu siku ile moja; hawakuwa wamevikwa kofia hii ya miiba vichwani mwao.

6. **Hatua ya sita: Math. 27: 27- 31,** Yesu pamoja na kuvikwa kofia ya miiba kichwani; sasa anabebeshwa ile nguzo nzito (**kg. 100)** begani na anaanza safari taratibu kuelekea (Golgotha!! Uzito wa ile nguzo pamoja na uchovu wa kupoteza damu nyingi unasababisha Yesu aanguke chini na kushindwa kabisa kuibeba ile nguzo!!!
***Math. 27: 32.* Akapigwa sana ili ainuke pale chini na kuubeba msalaba huu mzito maana walidhania kuwa amejifanya lakini alishindwa.**
7. **Hatua ya saba: 27: 33 – 38.** Walipofika Golgotha; ile nguzo aliyokuwa amebebeshwa Simon Mkrene inatuliwa chini; Yesu analazwa juu yake; mikono yake inanyooshwa kwenye mbao hizo na misumari mizito na mikubwa ya chuma inapigiliwa katika viganja vya mikono ya Yesu wakianzia na kiganja cha kulia na baadae kiganja cha kushoto; halafu nguzo hiyo inainuliwa, na ndipo miguu ya Yesu inayooshwa na kipande kikubwa cha chuma kinapigiliwa kwenye miguu ya Bwana Yesu. Yesu anapitia yote haya ili kulipa gharama ya dhambi zangu!!!
Haya yalikuwa ni mateso makali mno waliyofanyiwa majambazi sugu ili wengine wakiona hivi, waogope kabisa kujihusisha na wizi pamoja na unyanganyi!!! (Leo bado zipo nchi ambazo majambazi wanakatwa viganja vyote vya mikono kama adhabu ya kuwafanya wengine waogope kuiba/kunyanganya.

8. **Hatua ya nane: Math. 27: 39 – 40, Yesu sasa ni kama kituko (kioja) cha kutia/kuonea huruma, anachuruzika damu mwili mzima; amejaa majeraha mwili wote; yuko uchi hadharani; ana kofia ya miiba kichwani; badala asikie pole; mtu ambaye sasa anasikia kiu maana maji yametiririka na yameisha mwilini mwake; Yesu anasikia matusi/matukano!!! Anasikia dhihaka hata kwa wapita njia pamoja na wale aliowatendea mema!!!** ***Math. 27:39–44.*** Ndiyo sababu Yesu alipotiwa moyo na mhalifu mmoja alimwangalia kwa jicho la pekee sana saa hiyo hiyo. ***Luk.23: 39 – 43***

10. **<u>Hatua ya tisa: Math. 27: 45- 46</u>. <u>Yesu analia pale alipoona hata Mungu Baba amemuacha!!</u>**

- Kwa mara ya kwanza anaonja **kutengwa** na Mungu kama mbadala wa wenye dhambi. ***2Kor. 5: 21, Isay. 53:5, 1Pet. 1: 18 – 19.*** Huu ulikuwa ni wakati mgumu sana kwa Yesu kuliko nyakati zote za mateso yake; kwingine kote aliteswa akawa amenyamaza, ilipofika saa hii ya kuachwa na Mungu Baba, alilia!!! Eloi Eloi – ni lugha ya Kiyunani inayomaanisha kilio cha kukosa msaada toka popote!!! Akaona sasa amezungukwa na mauti, mapepo, majini, na kila aina ya nguvu za giza zinatamba jinsi zinavyotaka. Ndugu zangu, mashamublizi na mateso ya shetani kwa watu wasio na wokovu ni mabaya na yanatisha mno.

10. **<u>Hatua ya kumi: Math. 27: 50, Yoh. 19: 30</u>. Yesu akiwa katika mateso makali kuliko mateso mengine ya nyuma, ya kuonja maumivu na mateso yetu tunapokuwa Mungu ametuacha /ametutenga na shetani kufanya lolote analotaka kwetu; alilia kwa nguvu/alipaza sauti yake kwa nguvu" IMEKWISHA. (IT HIS FINISHED) Maana yake kazi ya ukombozi wetu ameimaliza kwa ukamilifu.**

- **Kilio hicho kinaashiria mwisho wa mateso yake yote kumalizika kwa kazi ya ukombozi wetu; deni la dhambi zetu zote likalipwa; hati zote za mashtaka yetu zikafutwa na kisha mpango kabambe wa wokovu wetu ukaanzishwa saa hiyo hiyo alipokata roho yake. *Math. 27: 50 – 54; Kol. 2: 13 – 15, Zab. 103: 1 – 5, Tito 3: 4-7***
- Pazia la hekalu kupasuka kuliashiria dhahiri tangu siku hiyo kwamba njia ya kila amwamiye Yesu; kwenda kwenye uwepo wa Mungu Baba na kuzungumza naye ni wazi kabisa. Zamani pazia la hekalu lilikuwa linazuia/linatenganisha kati ya patakatifu pa kawaida na Patakatifu pa Patakatifu
- Kupitia kifo cha Bwana Yesu, pazia liliondolewa na njia ya kila aaminiye kwenda mahali Patakatifu sana ikawekwa wazi kabisa. ***Ebr. 9: 1 – 14 na Ebr. 10: 19 – 22.***

"swali la kujiuliza kila mmoja – ***Ebr. 2: 3, 2Petr. 2: 20***; Gharama kubwa ililipwa kwa ajili yangu; Bwana nisaidie ili nijali neema hii, nisije nikawa kama mbwa asiye na akili au nguruwe nikaichezea tena neema hii. ***Amina***

***Na***
***Ask. Dr. L. M. Mwizarubi***
***PASAKA 2021***